



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI
SHIRIKA LA RELI TANZANIA**



**Simu: 2133990
Telegram: Railways
Nukushi: 2133428**

**Ofisi ya Uhusiano
S.L.P 76959
Barabara ya Sokoine
Dar es Salaam**

**TAARIFA KWA UMMA
YAH: AJALI YA TRENI ILIYOTOKEA MWANZA KUELEKEA DAR ES SALAAM**

Dar es Salaam, Tarehe 3 Mei 2023.

Shirika la Reli Tanzania – TRC linataarifu umma kutokea kwa ajali ya treni ya abiria yenye kichwa namba 9002 na mabehewa TCB4, FCB1, BVB1 iliyokuwa ikitokea mkoani Mwanza kuelekea Dar es Salaam alfajiri ya tarehe 3 Mei 2023 katika eneo kati ya Stesheni ya Fela na Mantare majira ya saa tisa usiku. Ajali hii imesababisha uharibifu wa miundombinu uliosababishwa na mvua zinazoendelea kunyeshwa nchini.

Treni hiyo ilibeba abiria 89 na wafanyakazi 16 wakitokea Mwanza kuelekea Dar es Salaam. Katika ajali hakuna majeruhi wala vifo vilivyotokea. Shirika limeshafanya utaratibu wa abiria kuendelea na safari.

Shirika la Reli Tanzania linaomba radhi kwa usumbufu uliojitokeza kwa abiria na linaendelea kufanya jitihada za kukabiliana na ajali zinazojitokeza kwa kujali usalama wa abiria na mizigo.

**Jamila Mbarouk
Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano**
